# Ukarabati uzio mnada wa Pugu wawekwa mkakati maalum

**Na Edward Kondela**

■■WAFANYABIASHARA katika Mnada wa Kimataifa wa Pugu uliopo jijini Dar es Salaam, wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kutatua changamoto zilizopo katika mnada huo ili uwe na tija kwao na taifa kwa ujumla.

Wakizungumza jana baada ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabirel kufika mnadani hapo, kwa ajili ya kufuatilia maelekezo ya uboreshaji aliyoyatoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki baada ya kufika mnadani hapo hivi karibuni, wamesema wana imani kuwa mnada huo ukiboreshwa zaidi utaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa.

Baadhi ya wafanyabiashara waliowasilisha kero zao kwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel wamesema bado wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao, uzio wa mnada kutokuwepo katika baadhi ya maeneo na kuchangia mifugo kutoka nje ya mnada hali ambayo inaweza kusababisha baadhi ya mifugo kupotea.

"Tatizo kubwa hapa kwenye mnada huu ni maji kwa ajili ya mifugo viongozi mbalimbali wamewahi kuja hapa pamoja na kuchimba kisima na kuwekwa birika la kunyweshea maji mifugo, lakini hakujawahi kuwepo maji hata siku moja ninashauri lirekebishwe lambo ambalo limekuwa likitumiwa siku nyingi tutakuwa na uhakika wa maji," alisema Said Waziri mmoja wa wadau katika mnada huo.

Aidha, baadhi ya wafanyabiashara hao walimuomba katibu mkuu huyo kuangalia uwezekano wa ukarabati wa barabara kutoka Gongo la Mboto ambayo inaelekea kwenye mnada huo ili magari yanayobeba mifugo yaweze kupita kwa urahisi kwa kuwa mifugo imekuwa ikipata majeraha na mingine kufa kutokana na kukanyagana wakati magari hayo yanapopita kwenye barabara hiyo ambayo ina mashimo makubwa.

Akizungumza mara baada ya kuwasikiliza wafanyabiashara hao Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel amesema wizara itafanya kila liwezekanalo ianze kufanya ukarabati wa uzio wa mnada kuanzia mwaka huu wa fedha 2020/21 na kuendelea na ukarabati katika bajeti ijayo ya mwaka fedha 2021/22.

Prof. Gabriel alisema suala la uzio wizara inalipa kipaumbele likisimamiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ili mnada huo wa kimataifa wa Pugu uweze kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara wa mnada huo.

"Nikiri kwamba pamoja na mambo mengine alichonituma waziri kuja kuangalia kwa umakini sana ni suala la uzio na tutaona jinsi gani ya kuanza kwa mwaka huu wa fedha na tutalianza mara moja na nimeshawaelekeza wataalamu waje kuangalia nini cha kufanya," alisema Prof. Gabriel.

Kuhusu changamoto ya ubovu wa barabara kutoka Gongo la Mboto hadi katika mnada huo, katibu mkuu huyo aliongea kwa njia ya simu akiwa mnadani hapo na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mhandisi Victor Seff, ambaye amesema atalisimamia suala hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Prof. Gabriel alisema kuhusu changamoto ya ukosefu wa maji, suala hilo analichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi na kutafuta njia ambayo itaweza kusaidia uwepo wa maji ya uhakika kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Pia, katibu mkuu huyo alielekeza kuanza kutumika mara moja kipakilio cha mifugo kwenye malori ambacho kimekamilika licha ya uwepo wa baadhi ya marekebisho ambayo ameelekeza yafanyiwe huku kikiendelea kutumika kutokana na wafanyabiashara kulalamika kupata wakati mgumu wakati wa kupakia na kushusha mifugo kwenye malori.

Kufuatia maelekezo hayo baadhi ya wafanyabiashara walisema wamefurahishwa na kauli zilizotolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel na kubainisha kuwa wamepata imani kubwa kwa wizara hiyo kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ili waweze kufanya shughuli zao katika mazingira rafiki zaidi.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel (mwenye fimbo) akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara wa mnada wa kimataifa wa Pugu uliopo jijini Dar es Salaam mara baada ya kusikiliza kero zao na kubainisha namna wizara ilivyojipanga kuziba maeneo yasiyo na uzio na kutatua kero za maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo. (Picha na Edward Kondela)

## Wakulima wa pamba Kishapu waishukuru Serikali

**Na Mwandishi Wetu, Shinyanga**

■■WAKULIMA wa zao la pamba wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wameishukuru Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dkt. John Magufuli kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapatia kwa mkopo dawa za kuulia wadudu waharibifu ambapo kwa sasa wataepukana na mikopo umiza waliyokuwa wakitozwa na watu binafsi.

Shukrani hivi karibuni na wanachama wa Chama cha Ushirika cha Msingi cha Kishapu (AMCOS) wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa viuadudu.

Wakulima hao walisema uamuzi wa Serikali kuanza kuwapatia viua wadudu kwa njia ya mkopo utaongeza ufanisi katika shughuli zao kilimo na hawatahangaika tena kutafuta viuatilifu hivyo kutoka kwa watu binafsi wanaowatoza riba kubwa na kusabisha washindwe kunufaika na kilimo chao.

Mmoja wa wakulima hao, Ally Mfaume alisema kitendo cha Serikali kuwakumbuka wakulima katika kuwapatia viua dudu hivi sasa changamoto ya ukosefu wa pembejeo haitakuwepo tena na wao watajikita katika kilimo na wataweza kupulizia mapema pamba yao dawa tofauti na msimu iliyopita.

"Mwanzo tulikuwa tunaingia mikataba na wafanyabiashara binafsi kwa sharti baada ya mavuno kuwalipa pamba mbegu.

Scanned with CamScanner

...ayokidhi mahitaji ya ...

JAMVI LA HABARI UK. 6 14 APRILI, 2021

# Wafanyabiashara waiomba serikali kutatua changamoyo za Pugu

NA EDWARD KONDELA

WAFANYABIASHARA katika Mnada wa Kimataifa wa Pugu uliopo jijini Dar es Salaam, wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kutatua changamoto zilizopo katika mnada huo ili uwe na tija kwao na taifa kwa ujumla.

Wakizungumza juzi baada ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabirel kufika mnadani hapo, kwa ajili ya kufuatilia maelekezo ya uboreshaji aliyoyatoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki baada ya kufika mnadani hapo hivi karibuni, wamesema wana imani kuwa mnada huo ukiboreshwa zaidi utaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa.

Baadhi ya wafanyabiashara waliowasilisha kero zao kwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel wamesema bado wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao, uzio wa mnada kutokuwepo katika baadhi ya maeneo na kuchangia mifugo kutoka nje ya mnada hali ambayo inaweza kusababisha baadhi ya mifugo kupotea.

"Tatizo kubwa hapa kwenye mnada huu ni maji kwa ajili ya mifugo viongozi mbalimbali wamewahi kuja hapa pamoja na kuchimba kisima na kuwekwa birika la kunywea maji mifugo, lakini hakujawahi kuwepo maji hata siku moja ninashauri litekebishwe lambo ambalo limekuwa likitumiwa siku nyingi tutakuwa na uhakika wa maji." Amesema Bw. Said Waziri mmoja wa wadau katika mnada huo.

Aidha, baadhi ya wafanyabiashara hao wamemuomba katibu mkuu huyo kuangalia uwezekano wa ukarabati wa barabara kutoka Gongo la Mboto ambayo inaelekea kwenye mnada huo ili magari yanayobeba mifugo yaweze kupita kwa urahisi kwa kuwa mifugo imekuwa ikipata majeraha na mingine kufa kutokana na kukanyagana wakati magari hayo yanapopita kwenye barabara hiyo ambayo ina mashimo makubwa.

Akizungumza mara baada ya kuwasikiliza wafanyabiashara hao Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Profesa Elisante Ole Gabriel amesema wizara itafanya kila liwezekanalo ianze kufanya ukarabati wa uzio wa mnada kuanzia mwaka huu wa fedha 2020/21 na kuendelea na ukarabati katika bajeti ijayo ya mwaka fedha 2021/22.

Profesa Gabriel amesema suala la uzio wizara inalipa kipaumbele likisimamiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki ili mnada huo wa kimataifa wa Pugu uweze kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara wa mnada huo.

"Nikiri kwamba pamoja na mambo mengine alichonituma waziri kuja kuangalia kwa umakini sana ni suala la uzio na tutaona jinsi gani ya kuanza kwa mwaka huu wa fedha na tutalianza mara moja na nimeshawaelekeza wataalamu waje kuangalia nini cha kufanya." Amesema Prof. Gabriel

Kuhusu changamoto ya ubovu wa barabara kutoka Gongo la Mboto hadi katika mnada huo, katibu mkuu huyo ameongea kwa njia ya simu akiwa mnadani hapo na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mhandisi Victor Seff, ambaye amesema atalisimamia suala hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Prof. Gabriel amesema kuhusu changamoto ya ukosefu wa maji, suala hilo analichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi na kutafuta njia ambayo itaweza kusaidia uwepo wa maji ya uhakika kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Pia, katibu mkuu huyo ameelekeza kuanza kutumika mara moja kipakilio cha mifugo kwenye malori ambacho kimekamilika licha ya uwepo wa baadhi ya marekebisho ambayo ameelekeza yafanyiwe huku kikiendelea kutumika kutokana na wafanyabiashara kulalamika kupata wakati mgumu wakati wa kupakia na kushusha mifugo kwenye malori.

Kufuatia maelekezo hayo baadhi ya wafanyabiashara wamesema wamefurahishwa na kauli zilizotolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel na kubainisha kuwa wamepata imani kubwa kwa wizara hiyo kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ili waweze kufanya shughuli zao katika mazingira rafiki zaidi.

Scanned with CamScanner

# Skin factories: Ministry proposes sharp tax cuts

FROM PAGE 1

about 80m/- per unit, with traders blaming taxes on importing such units, meanwhile as low investment in value addition prunes earnings substantially by exporting raw hides and skins.

Tanzania is the second in livestock numbers in Africa, accounting for 11 per cent of African cattle population, while the contribution of the leather sector to GDP is statistically minimal, experts say.

Critics say low public financing in budget allocation is the problem, but others point at low capitalisation of the sector, anchored in traditional livestock keeping on communal lands hindering credit flows to build factories or acquire modern technology.

Last year, the government launched the Tanzania Livestock Master Plan (TLMP) to address major challenges facing the sector as part of the Tanzania Development Vision (TDV) towards 2025, projecting a livestock sector that is commercially run, modern and sustainable.

It is expected to be using improved and highly productive livestock to ensure food security, improved income for households and the nation while conserving the environment, all of which is inconsistent with current grazing land occupancy and rearing structures..

However, the trend setting Analysis of Public Financing on the Livestock Sector, a study by civil society organizations, shows that for the last six fiscal years, Tanzanian national budget has been increasing at consistently high rates, and thus its capacity to finance various sectors.

It rose by 15bn/- in the fiscal year 2012/13 and over 31bn/- in fiscal 2017/18, where the total budget doubled from fiscal 2012/13 to fiscal 2017/18, while public agricultural sector financing did not exceed seven percent.

Government commitment to the Maputo and Malabo declarations implies it adheres to 10 percent national budget allocation to the agriculture sector to attain annual 6 percent sector net growth, CSOs emphasise

Scanned with CamScanner

# Skin factories: Ministry proposes sharp tax cuts

By Correspondent James Kandoya

POLICY shift is evident at the Ministry of Livestock and Fisheries as it is seeking a 50 per cent tax cut on imported leather processing machines as part of efforts to rescue large parts of 98 per cent of skins that go to waste due to poor quality.

Speaking to The Guardian in an interview yesterday, minister Mashimba Ndaki said the ministry has already reached out to the Treasury to slash the specific taxes by half to enable more Tanzanians to set up skin processing factories.

"There are few such machines in the country due to tax added costs. Iit is our hope that by cutting taxes by half many people will afford the machines and improve quality in the skin sub-sector," he said, expressing the hope that the proposal will be examined and included in tax proposals during the ongoing parliamentary budget session.

The livestock sector is predominantly made of smallholder keepers and pastoralists, overly subsistent in character and lacking access to modernised inputs, professional services as well as adequate information on opportunities in the sector and produce markets.

.Anna Malongo (25), a shoe maker in Nkunhungu suburb of Dodoma said that high pricing of the machines compels fabric makers to use manual types of tools that consume more energy and time to make a product, underlining that with more skin processing plants shoe makers would do a better business and cut prices of shoes.

Local leather dealers say that leather tanning and processing machines cost is

TURN TO PAGE 2

9 770856 542009 >

The Guardian Uk.1-2
14 Aprili, 2021

Scanned with CamScanner